

Maswali

1. Mbona Mungu alikasirikia Waisraeli?
2. Waisraeli walinun'gunikia nini?
3. Mungu alitumia Waisraeli adhabu gani?
4. Nini ilifanyika wakati Waisraeli waliumwa na nyoka za moto?
5. Waisraeli waliuliza Musa afanye nini?
6. Mungu aliondoa wale nyoka?
7. Mungu alisema atafanya nini tena?
8. Mungu aliambia Musa atengeneze nini?
9. Waisraeli waliponywa namna gani?
10. Mungu anatufunza somo gani kuhuzu Yesu?

Majibu

1. Mungu alikasirika kwa sababu Waisraeli walikuwa wananun'gunika tena.
2. Njia ilikuwa ngumu, walitaka maji mengi tena walichoka na mana.
3. Mungu alitumia nyoka za moto kama adhabu kwa Waisraeli.
4. Walikuwa wagonjwa, na maumivu tena walikufa.
5. Waisraeli waliuliza Musa awaombee kwa Mungu.
6. Ndiyo, Mungu aliondoa nyoka za moto.
7. Mungu alisema ataponya watu walioumwa.
8. Mungu aliambia Musa atengeneze nyoka ya shaba kwa mti.
9. Waisraeli waliponywa kwa kuamini Mungu na kuangalia nyoka.
10. Yesu aliinuliwa msalabani, ili tukiamini na kutii Mungu tutaokoka.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 1



25 Nyoka ya shaba

Kwa Biblia Hesabu 21:4-9; Yohana 3:14-16

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu aliokoa watu wake walipokuwa na imani.

Somo

Waisraeli walisafiri jangwani. Walitoka jangwani na kukwea miamba iliyokuwa kando ya Bahari ya Shamu. Lakini baadaye Waisraeli walichoka na wakanun'gunikia Musa. Walisema njia hiyo ilikuwa ngumu sana kwao.

Tena Waisraeli walinun'gunika kwamba hawakukuwa na maji ya kutosha. Walisema wamechoka kukula mana iliyotumwa na Mungu kila siku. Walisema, Misri walikuwa na vyakula vingi tofauti vya kukula. Walitamani kurudi Misri.

Mungu alikasirikia na Waisraeli. Alikuwa amewaokoa kutoka Misri. Aliwalinda safarini wakati walikuwa huko jangwani. Mungu aliwapa maji ya kunywa. Aliwatumia mana ya kukula kila asubuhi. Lakini Waisraeli hawakukuwa na shukrani kwa Mungu. Hawakuamani Mungu. Walikuwa wakinun'gunika mara tu mambo yalipoenda mrama.

Mungu alituma nyoka za moto kambini. Nyoka za moto zilitokezea ghafula. Waisraeli walipiga mayowe wakitorokea kwa mahema. Lakini nyoka walijinyonganyonga na kuenda hemani. Nyoka waliuma watu. Nyoka wenyewe walikuwa wa sumu na watu wengi walikufa.


Watu wengi walilala kwa mahema wakiwa wagonjwa sana kwa kuumwa na nyoka. Walikuwa na uchungu sana wa kuumwa. Kila mtu aliogopa. Hawakujua wakati nyoka watakuja na kuwauma. Kambini kulikuwa na kuugua na kulia kwa hofu. Waisraeli walikuwa na uoga sana. Kambini, nyoka za moto walikuwa kila mahali. Waliendelea kuwauma



Waisraeli waliendea Musa. Walisema, "Tumefanya dhambi. Tulikosa kunun'gunika. Tafadhali tuombe, uuliza Mungu atusamehe. Tafadhali ambia Mungu aondoe hawa nyoka za moto."

Musa aliomba Mungu. Mungu alisikia Musa na akaondoa nyoka za moto. Lakini kulikuwa na watu wengi waliokuwa bado wagonjwa sana kwa kuumwa na nyoka. Mungu alikuwa na huruma. Alisema atawatibu. Mungu alimwambia Musa atengeneze mfano wa nyoka kutoka kwa shaba na aiweke juu ya mti. Mungu aliwambia kwamba yeyote atakae angalia nyoka ya shaba atapona kutokana na kuumwa na nyoka.

Musa alitengeneza nyoka ya shaba haraka sana. Aliiweka juu kwa mti. Musa aliambia Waisraeli kwamba Mungu ataponya wote waliokuwa wagonjwa kwa kuumwa na nyoka. Musa aliwambia kwamba kila mtu aliyeumwa lazima aangalie nyoka ya shaba mtini. Wakiangalia nyoka ya shaba watapona. Musa aliweka nyoka ya shaba kwa mti juu sana penye kila mtu angeona.



Waisraeli wengi walikuwa wameumwa na nyoka za moto. Walikuwa wagonjwa sana. Walikuwa kwa maumivu nyingi. Lakini waliamini kwamba Mungu atawaponya. Walijaribu kutoka kwa vitanda ili wawe nje ya hema. Waliangalia nyoka ya shaba mtini. Walipoangalia nyoka ya shaba, walipona.

Waisraeli wengine hawakuamini kwamba watapona wakiangalia nyoka ya shaba. Hawakujaribu kuamka na watoke nje ya hema. Watu hawa walikufa kwa ajili ya kuumwa na nyoka.

Nyoka ya shaba haikukuwa ya uchawi au muujiza. Nyoka ya shaba ilikuwa ni kipande cha chuma tu. Haingeweza kuponya yeyote. Mungu ndiye aliponya watu. Lakini ilikuwa lazima watu waamini na kutii Mungu ndio waponywe.


Mungu ako anatufundisha somo kwa hii hadithi ya nyoka ya shaba. Ako anatufundisha somo juu ya Yesu. Nyoka ya shaba iliinuliwa juu ya mti. Kila mtu aliyeamini na kuiangalia hakukufa. Walipona na kuishi. Yesu aliinuliwa juu kwa msalaba. Kila mtu aaminiye Yesu na kutii Mungu hatakufa kamwe. Atakuwa na uzima wa milele.

Nyoka ya shaba



Ilinuliwa juu ya mti
Watu walitakiwa waamini
na kutii Mungu
Halafu walipona na kuokoa
maisha yao

Yesu



Aliinuliwa juu kwa msalaba
Tuwe na imani kwa Yesu
na kutii Mungu
Tutaokoka na kuwa na
uzima wa milele